TANGAZO LA SERIKALI NA. 209 la tarehe 22/3/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 8(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MAEGESHO NA VITUO VYA VYOMBO VYA USAFIRI YA HALMASHAURI YA MJI MAFINGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Mafinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Mafinga;

"karakana" maana yake ni eneo la Halmashauri lililotengwa au litakalotengwa kwa ajili ya shughuli za ufundi na kuhifadhi vyombo vya usafiri;

"kituo" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya maegesho au kwa ajili ya huduma za usafiri ambapo vyombo vya usafiri vitapakia au kushusha abiria au mizigo;

"maegesho" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili yya kuegesha vyombo vya usafiri;

"maegesho yaliyohifadhiwa" maana yake ni maeneo maalumu yaliyotengwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya maegesho binafsi ya vyombo vya usafiri kwa ajili ya mtu binafsi au taasisi;

"stendi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru wa stendi" maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na Halmashauri kwa vyombo vya usafiri vinavyoingia stendi au mtu yoyote anayefanya shughuli katika stendi;

"vituo vya njiani" maana yake ni vituo vyote vilivyopo pembeni ya barabara vinavyotumika kupakia na kushusha abiria ambavyo si stendi;

"wakala" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Halmashauri kutekeleza majukumu chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Ushuru wa maegesho

4.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa vyombo vyote vya usafiri kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Mtu mwenye chombo cha usafiri kinachoingia katika eneo lolote la maegesho atalipa ushuru wa maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1) na (2), vyombo vya usafiri vinavyomilikiliwa na Serikali, wanadiplomasia, majeshi na magari ya kubeba wagonjwa havitatozwa ushuru wa maegesho.

Maeneo ya maegesho

5.-(1) Kituo Kikuu cha mabasi, kituo cha kuegesha magari ya mizigo na maeneo mengine yaliyotengwa au yatakayotengwa na Halmashauri kama maeneo ya maegesho yatakuwa ni vituo vya maegesho.

(2) Halmashauri inaweza kugawa maeneo ya maegesho kwa mistari au kwa kutumia alama yoyote itakayoonyesha idadi na sehemu ambayo chombo cha usafiri kinatakiwa kuegeshwa.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (2), kukosekana kwa mistari au alama za maegesho hakutaathiri madai ya ada ya maegesho ya chombo cha usafiri kilichoegeshwa ndani ya maeneo hayo.

Uanzishaji wa vituo vya vyombo vya usafiri

6. Halmashauri inaweza kuanzisha vituo vya vyombo vya usafiri wa umma vinavyotoa huduma ndani ya Halmashauri, vinavyotoka nje ya Halmashauri na vinavyoingia ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

Utaratibu wa kutumia vituo vya vyombo vya usafiri

7.-(1) Mtu anayeendesha chombo cha usafiri wa umma hatapakia au kushusha abiria au mizigo nje ya kituo au stendi.

(2) Safari zote za mabasi zitaanzia na kumalizika katika stendi ya mabasi isipokua kwa mabasi yanayopita kutoka na kuelekea maeneo mengine ya nje ya Halmashauri.

(3) Chombo cha usafiri wa umma hakitasimama kwa zaidi ya dakika tano katika vituo vya njiani.

(4) Mtu hatafanya matengenezo au kuosha chombo cha usafiri katika kituo au stendi isipokuwa kwa idhini ya Halmashauri.

(5) Mtumiaji wa kituo au stendi hatatumia lugha ya matusi, inayoweza kuleta uchochezi, bughudha au inayoweza kuhatarisha usalama na amani ndani ya kituo.

Maegesho yaliyohifadhiwa

8.-(1) Baada ya kupokea maombi kutoka kwa mtu yeyote anayetaka kutengewa eneo la kuegesha chombo cha usafiri, Halmashauri inaweza kutenga eneo la maegesho kuwa ni maegesho yaliyohifadhiwa.

(2) Katika kushughulikia maombi chini ya aya hii, Halmashauri itazingatia yafuatayo:

(a) athari kwa biashara au shughuli katika eneo husika endapo kibali hicho kitatolewa;
(b) uwepo wa maegesho katika eneo hilo;
(c) uwepo wa eneo mbadala la maegesho;
(d) idadi ya maeneo au nafasi zinazoombwa kuhifadhiwa; na
(e) iwapo muda uliopendekezwa kwa ajili ya eneo hilo kuhifadhiwa unafaa.

(3) Endapo maombi yatakataliwa, Halmashauri itamtaarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataliwa.

(4) Endapo maombi yatakubaliwa na mwombaji kulipa ushuru wa maegesho, ataruhusiwa kutumia sehemu hiyo yeye peke yake bila ya kuingiliwa.

Maegesho yasiyo rasmi

9.-(1) Mtu hataegesha chombo chochote cha usafiri katika maeneo yasiyo rasmi kwa ajili ya maegesho au kuegesha kwa namna isiyoruhusiwa.

(2) Halmashauri inaweza kuzuia kwa kufunga vifaa maalumu kwenye chombo cha usafiri kilichoegeshwa vibaya au kilichoegeshwa katika eneo lisiloruhusiwa na kumtaka mmiliki au mtumiaji kulipa faini kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(3) Chombo cha usafiri kilichozuiwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (2) kwa zaidi ya saa mbili bila ya kulipiwa

kitavutwa na kupelekwa katika karakana iliyoidhinishwa na Halmashauri kwa gharama za mmiliki wa chombo hicho na Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu utakaotokea wakati wa uvutwaji huo.

Chombo cha usafiri kilichotelekezwa

10.-(1) Chombo cha usafiri ambacho kitahifadhiwa katika karakana kwa muda wa siku thelathini bila kukombolewa, kitachukuliwa kuwa kimetelekezwa.

(2) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita Halmashauri inaweza kupeleka maombi mahakamani ili iweze kutamka kuwa chombo hicho kimetelekezwa na kutoa kibali chombo hicho kiuzwe kwa njia ya mnada wa hadhara.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (2), kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa notisi ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza chombo hicho.

(3) Fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya chombo cha usafiri zitatumika kulipa ushuru unaodaiwa, pamoja na gharama za kukamata na fedha zitakazobaki zitarejeshwa kwa mmiliki au mwakilishi wake.

Maegesho kwa muda maalumu

11. Magari makubwa ya mizigo yenye zaidi ya tani tano hayataegeshwa katikati ya mji isipokuwa kwa kibali maalumu na kilipiwa ada iliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Usajili wa teksi, bajaji na pikipiki

12.-(1) Mmiliki wa teksi, bajaji au pikipiki inayofanya kazi ndani ya Halmashauri atasajili kwa Halmashauri na kulipia ada ya usajili ya chombo hicho cha usafiri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoa stika za usajili wa teksi, bajaji au pikipiki kwa kila mmiliki, na itakuwa wajibu wa kila mmiliki kubandika stika atakayopewa na Halmashauri pembeni mwa chombo chake cha usafiri.

Ukusanyaj

13. Ushuru wa vyombo vya usafiri utakusanywa kwa

i wa ushuru wa vyombo vya usafiri

mujibu wa Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

14. Afisa mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri ambacho kimeegeshwa katika maeneo yasiyo rasmi kwa ajili ya maegesho au kuegeshwa kwa namna isiyoruhusiwa.

Makosa

15. Mtu anatenda kosa endapo mtu huyo-

(a) anakataa au anashindwa kulipa ushuru wa maegesho;
(b) anamshawishi mtu yeyote au kundi la watu kukataa kulipa ushuru wa maegesho;
(c) anapakia au anashusha abiria au mizigo katika eneo ambalo ambalo nje ya kituo au stendi;
(d) anafanya matengenezo au kuosha gari katika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya maegesho;
(e) anaegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo halijaruhusiwa;
(f) anakataa kutoa taarifa au atatoa taarifa za uongo kwa Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala pale zitakapohitajika;
(g) anaanzisha eneo la maegesho yaliyohifadhiwa bila idhini ya Halmashauri; au
(h) anaegesha chombo cha usafiri nje ya mstari uliochorwa kuainisha eneo la kuegeshea chombo cha usafiri.

Adhabu

16. Mtu anayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Ufifilishaji makosa

17. Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kulipa kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi katika fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

USHURU WA VYOMBO VYA USAFIRI NA HUDUMA KATIKA STENDI, VITUO NA MAEGESHO

(a) Ushuru wa kuingia stendi

| Namba. | Aina ya Chombo | Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi dogo la abiria kati ya 1 – 20 | 1,000 kwa siku |
| 2. | Basi kubwa la abiria kati ya 20 – 28 | 1,000 kwa siku |
| 3. | Basi kubwa la abiria zaidi ya 28 | 3,000 kwa siku |
| 4. | Teksi iliyosajiriwa kufanya kazi stendi | 1,000 kwa siku |
| 5. | Gari dogo binafsi linaloingia na kutoka | 500 kila inapoingia |
| 6. | Magari ya mizigo | 1,000 kila inapoingia |
| 7. | Pikipiki | 500 kila inapoingia |
| 8. | Bajaji | 500 kila inapoingia |
| 9. | Magari mengineyo | 1,000 kila inapoingia |
| 10. | Ada ya kuingia mtu mmoja | 200 kila inapoingia |
| 11. | Teksi anayoshusha abiria na kuondoka | 500 kila inapoingia |
| 12. | Huduma ya kutumia choo Stendi na maeneo mengine ya Halmashauri | 200 kila unapopata huduma |
| | | 500 kwa huduma ya kuoga |
| 13. | Ada ya kutunza gari lililo kamatwa au kuzuiliwa | 10,000/= |

(b) Ushuru kulaza chombo cha usafiri stendi

| Namba. | Aina ya Chombo | Ushuru wa kulaza chombo cha usafiri kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria kati ya 20-28 | 5,000 |
| 2. | Basi kubwa la abiria 28 | 8,000 |
| 3. | Basi dogo la abiria kati ya 1-20 | 4,000 |
| 4. | Teksi | 2,000 |

*Tangazo La Serikali Na. 209 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Gari dogo binafsi | 2,000 |
| 6. | Gari ya mizigo yenye uzito usiozidi tani 3 | 5,000 |
| 7. | Gari ya mizigo yenye uzito unaozidi tani 3 | 10,000 |
| 8. | Magari ya mizigo | 4,000 |
| 9. | Magari mengine | 4,000 |
| 10. | Pikipiki | 1,000 |

(c) Ushuru wa maegesho

| Namba | Aina ya Gari | Ushuru (Shilingi) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kwa saa | Kwa siku | Kulaza gari/siku |
| 1 | Gari ya mizigo zaidi ya tani 5 | 2,000 | 3,000 | 5,000 |
| 2 | Gari la mizigo chini ya tani 5 | 1,000 | 2,000 | 3,000 |
| 3 | Pick up/station wagon | 1,000 | 2,000 | 3,000 |
| 4 | Lori lenye trela isiyozidi tani 3 | 1,000 | 2,000 | 3,000 |
| 5 | Lori lenye trela tani 3 na zaidi | 2,000 | 3,000 | 5,000 |
| 6 | Gari la abiria (nje ya stendi) | 1,000 | 2,000 | 5,000 |
| 7 | Gari dogo binafsi | 500 | 1,000 | 2,000 |
| 8 | Bajaji | 200 | 500 | 1,000 |
| 9 | Pikipiki | 200 | 300 | 1,000 |
| 10 | Mitambo na magari mengine | 1,000 | 2,000 | 4,000 |

---

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 17)*

### FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi....................................................................nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ...................................................................ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga, kwamba mnamo tarehe..........ya mwezi.......................Mwaka...........................nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya...............ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Nipo tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

Ninathibitisha kuwa maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu na kadri ya ufahamu wangu.

Leo tarehe.....................ya Mwezi.........................Mwaka......................................

Jina................................................... Saini.............................................................

*Tangazo La Serikali Na. 209 (Linaendelea)*

MBELE YA:
Jina:......................................................
Wadhifa:...................................................
Saini........................................................
Tarehe.......................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Mafinga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Mafinga uliofanyika Tarehe 14 mwezi 02 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya ;-

AYUBU J. KAMBI
*Mkurugenzi*

REGNANT Z. KIVINGE

*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji Mafinga*

NAKUBALI

**L.S**

DODOMA
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*